SWALI: Katika *Ezra 9:12 na Kumbukumbu 7:3*, Tunaona Bwana Mungu aliwakataza waisraeli kuoana na watu wa mataifa. Je watumishi hawa walioolewa au kuoa mataifa walifanya dhambi?.

1. Esta kuolewa na mfalme Ahasuero

2. Boazi kumwoa Ruthu

3. Musa kumwoa Sipora, Mkushi,

Na kama ni dhambi mbona Miriamu Mungu alimpiga kwa ukoma baada ya kuhoji kwanini kaka yake, Musa alioa mwanamke wa kimataifa?

---

Jibu: Esta hakufanya jambo lililo sahihi kuolewa na mfalme wa kimataifa asiyemjua Mungu wa Israeli, kulingana na sheria za Mungu, lakini Mungu aliruhusu jambo hilo litokee,  kwa makusudi maalumu, kwamba Esta aolewe na Mfalme Ahasuero *(ambaye ni mtu wa kimataifa)* ili Mungu awaokoe watu wake dhidi ya maadui zao.

Utaona jambo kama hilo hilo lilitokea wakati wa Samsoni, pale

ambapo Samsoni alikuwa ni Mwisraeli lakini akaenda kutafuta kuoa wanawake wa kimataifa *(wakina Delila*). Utaona walikuwepo wanawake wengi wa kiisraeli wenye sifa zote, lakini Samsoni hakwenda kwa hao bali kwa Delila aliyekuwa mfilisti, na biblia inasema jambo lile lilitoka kwa Bwana. *(Yaani Mungu aliruhusu liwe hivyo)*

Waamuzi 14:3 "Ndipo baba yake na mama yake wakamwambia, Je! Hapana mwanamke hata mmoja katika ndugu zako, au katika jamaa zangu zote, hata uende kumwoa mwanamke kwa hawa Wafilisti wasiotahiriwa? Samsoni akamwambia baba yake; Mnipatie huyo, kwa maana ananipendeza sana.

> *4 Lakini baba yake na mama yake HAWAKUJUA YA KUWA JAMBO HILI NI LA BWANA; MAANA ALITAKA KISA JUU YA WAFILISTI. Basi wakati ule Wafilisti walikuwa wakiwatawala Israeli".*

Unaona?..Mungu aliruhusu Samsoni atafute mke wa kimataifa, ili tu kutafuta kisa cha kuwaokoa waisraeli watu wake, chini ya utawala wa wafilisti.

Na ndio hivyo hivyo kwa Esta, Mungu aliruhusu Esta aolewe na mwanaume wa kimataifa (Mfalme Ahasuero), lengo na madhumuni ni kutafuta tu kisa cha kuwaokoa Israeli dhidi ya maadui zao ambao walikuwa wanawanyanyasa chini ya utawala huo. Na kilipopatikana kisa, Maadui za Israeli wote walikufa na Israeli wakapata raha. Lakini hayakuwa mapenzi kamili ya Mungu, Esta aolewe na mwanaume wa kimataifa, wala Samsoni aoe mwanamke wa kimataifa, ilikuwa ni kinyume cha sheria za Mungu.

Lakini pamoja na hayo tunaona pia mtu mwingine akioa mke wa kimataifa, na huyo si mwingine zaidi ya Boazi, aliyemwoa Ruthu, aliyekuwa mwanamke wa kimataifa.

Sasa ni kwanini iwe hivyo?

Ni kwasababu Ruthu tayari alikuwa ameshaacha miungu ya kwao, na kumgeukia Mungu wa kweli wa Israeli, kwasababu lengo kuu la Mungu kuwaambia wana wa Israeli wasioe wanawake wa mataifa ni kuepuka kugeuzwa mioyo. *(1Wafalme 11:2)*. Na si lengo lingine.

Hivyo  Ruthu tayari alikuwa ameshaiacha miungu ya kwao, na

amemgeukia Mungu wa kweli wa Israeli kwa moyo wake wote, tofauti na Delila au Mfalme Ahasuero aliyemwoa Esta, hao walikuwa bado hawajaiacha miungu yao.

> *Ruthu 1:16  "Naye Ruthu akasema, Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, Na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu;*
>
> *17 Pale utakapokufa nitakufa nami, Na papo hapo nitazikwa; Bwana anitende vivyo na kuzidi, Ila kufa tu kutatutenga wewe nami".*

Kwahiyo unaweza kuona, Ruthu tayari moyo wake ulikuwa umeshahamia kwa Mungu wa Israeli, akili yake yote ilikuwa inamwaza Mungu wa Israeli, na watu wa Israeli, na kwa Imani hiyo akahesabika kuwa kama mmojawapo wa mwanamke wa kiisraeli, japokuwa ni mwanamke wa kimataifa.

Sawa  tu na yule Rahabu kahaba, ambaye naye pia kwa Imani, alihesabiwa kuwa mwanamke wa kiisraeli, ingawa alikuwa ni Myeriko, kwasababu aliiacha miungu ya kwao na kumwamini

Mungu wa Israeli na kumkiri.

> *Yoshua 2: 11 “Na mara tuliposikia hayo mioyo yetu iliyeyuka, wala haukusalia ujasiri wo wote katika mtu awaye yote, kwa sababu yenu; kwa kuwa Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu, katika mbingu juu na katika nchi chini”*

> *Waebrania 11: 30  “Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba*
>
> *31  Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani”..*

Na swali la mwisho ni kwanini Musa alimwoa Siphora, mkushi? Na ilihali yeye ni myahudi?

Kumbuka sheria ililetwa na Mungu kwa mkono wa Musa, hivyo Musa tayari alikuwa ameshaoa kabla ya hiyo sheria kuja. Kwahiyo haikuwa sahihi kumwacha mke wake huyo wa kimataifa na kuoa

mwingine ilihali ameshapata naye watoto. Hivyo Mungu alimbariki na huyo huyo mkewe, maadamu alikuwa naye pia anamcha Mungu wa Israeli. Na sio tu Musa peke yake aliyekuwa na mke wa kimataifa, bali hata Yusufu, biblia inasema mke wake alikuwa ni binti wa kuhani  wa Oni (Mwanzo 41:45), ambaye hakuwa myahudi. Lakini Mungu hakumpa maagizo amwache, kwasababu sheria hiyo bado ilikuwa haijaja.

Na sisi wakristo wa agano jipya, hatupaswi kuoa, wala kuolewa na mtu ambaye hajamkabidhi Yesu maisha yake (Mpagani), hiyo ni kulingana na maandiko. Ni sharti kwanza awe amemwamini Yesu na kusimama katika imani ndipo ndoa ifuate. (kwa urefu juu ya somo hili unaweza kufungua hapa >>  Je Ni sahihi kuolewa/kuoa mtu wa imani nyingine?)

Bwana akubariki.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya

Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo.

---

Mada Nyinginezo:

> *Je! Ni halali kuoa/kuolewa na mtu ambaye tayari anao watoto?*

> *Je! Ni sahihi kuoa/kuolewa na mtu uliyemzidi umri?*

> *JIFUNZE KUELEWA MAANA YA KUOA/KUOLEWA KABLA YA KUINGIA HUKO.*

> *Je! Ni sahihi kwa mkristo kuoa/kuolewa na mtu wa imani nyingine?*

> *JE NI HALALI KUOA WAKE WENGI, AU KUTOA TALAKA?*

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp